# WIZARA YA UCHUKUZI

# CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI

# SIFA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA MUDA MFUPI

**1. MAELEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO**

i. Mwombaji wa mafunzo anatakiwa akidhi vigezo kama ilivyoainishwa kwenye sifa za kujiunga na atalipia 20,000/= kupitia namba ya kumbukumbu ya malipo “control number” atakayopatiwa chuoni kwa ajili ya mtihani wa awali wa udereva.

ii. Malipo hufanyika siku za kazi na mtihani hufanyika kila siku za jumamosi kuanzia saa tatu (3) asubuhi.

iii. Zoezi la kujisajili kwenye mafunzo litafungwa ndani ya siku moja baada ya mafunzo kuanza.

iv. Mwombaji ni lazima awe na kitambulisho cha Taifa – NIDA.

v. Mwombaji ni lazima awe na uwezo wa kuendesha gari yenye mfumo wa “manual”

**2. SIFA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UDEREVA**

**i. MAFUNZO YA UDEREVA DARAJA LA PILI (ADVANCED DRIVERS GRADE II - VIP)**

a) Awe na elimu ya msingi au zaidi na aweze kusoma na kuandika.
b) Awe na leseni hai Daraja D ambayo ameifanyia kazi miaka mitatu na kuendelea.
c) Awe amefaulu mtihani wa awali wa udereva (pre driving test)

**ii. MAFUNZO YA UDEREVA DARAJA LA KWANZA (ADVANCED DRIVERS GRADE I)**

a) Awe na leseni hai
b) Awe na cheti cha udereva Daraja la pili kutoka NIT.

**iii. MAFUNZO YA UDEREVA MWANDAMIZI (SENIOR DRIVER)**

a) Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
b) Awe na cheti cha udereva Daraja la kwanza kutoka NIT.

**iv. MAFUNZO YA UDEREVA WA MAGARI YA ABIRIA (PSV – C)**

a) Awe na elimu ya msingi au zaidi na aweze kusoma na kuandika.
b) Awe na leseni hai Daraja E au C1 ambayo ameifanyia kazi kwa miaka mitatu.
c) Awe na umri usiopungua miaka 24.
d) Awe amefaulu mtihani wa awali wa udereva (pre driving test).

v. **MAFUNZO YA UDEREVA WA MAGARI YA ABIRIA (PSV – C 1)**

a) Awe na elimu ya msingi au zaidi na aweze kusoma na kuandika.
b) Awe na leseni hai Daraja D ambayo ameifanyia kazi kwa miaka mitatu.
c) Awe na umri usiopungua miaka 21.
d) Awe amefaulu mtihani wa awali wa udereva (pre driving test)

**vi. MAFUNZO YA UDEREVA WA MAGARI YA ABIRIA (PSV – C 2 NA C 3)**

a) Awe na elimu ya msingi au zaidi na aweze kusoma na kuandika.
b) Awe na leseni hai Daraja D ambayo ameifanyia kazi kwa miaka mitatu.
c) Awe na umri usiopungua miaka 21.
d) Awe amefaulu mtihani wa awali wa udereva (pre driving test)

(Mafunzo haya yataendeshwa pale ambapo kutakua na maombi maalum)

**vii. MAFUNZO YA MAGARI MAKUBWA YA MIZIGO (HGV)**

a) Awe na elimu ya msingi au zaidi na aweze kusoma na kuandika.
b) Awe na leseni hai ya kuendeshea gari Daraja E ambayo ameifanyia kazi kwa mwaka mmoja.
c) Awe na umri usiopungua miaka 21.
d) Awe amefaulu mtihani wa awali wa udereva (pre driving test).
e) Awe na vifaa vya usalama atakavyovitumia wakati wa mafunzo (kiatu cha usalama “safety boots”, kofia ngumu na reflecting vest)

**viii. MAFUNZO YA UDEREVA WA MAGARI YAENDAYO KWA HARAKA (BRT)**

a) Awe na leseni hai Daraja C.
b) Awe na cheti cha PSV kutoka chuo kinachotambulika na mamlaka husika.

**ix. MAFUNZO YA UENDESHAJI FORKLIFT**

a) Awe na leseni hai Daraja D
b) Awe na vifaa vya usalama atavyovitumia wakati wa mafunzo (kiatu cha usalama “safety boots”, kofia ngumu na reflecting vest)

**x. MAFUNZO YA WAKUFUNZI WA MADEREVA (DRIVER INSTRUCTOR COURSE)**

a) Awe na leseni hai yenye Daraja mojawapo au zaidi kati ya (C1, C au E) ambayo ameifanyia kazi kwa miaka isiyopungua mitatu.
b) Awe na cheti cha udereva mahiri kutoka katika chuo au taasisi inayotambulika.
c) Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
d) Awe na uwezo wa kuongea na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza.
e) Awe amefaulu mtihani wa awali wa udereva (pre driving test).

**xi. MAFUNZO YA AWALI YA UDEREVA (BASIC DRIVING)**

a) Awe na kitambulisho cha taifa – NIDA
b) Awe na leseni ya kujifunzia.

## 3. SIFA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA WAHUDUMU

**I. MAFUNZO YA WAHUDUMU WA MABASI (BPCS)**

a) Awe na kitambulisho cha taifa – NIDA
b) Awe anajua kusoma na kuandika